

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

01

KISWAHILI

Muda: Saa 1:30

MAJIBU

Mwaka: 2021

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika majibu yote kwenye nafasi zilizoachwa wazi katika kila swali.
4. Andika majibu yote kwa kutumia kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi**

maktaba.tetea.org



SEHEMU A: (Alama 10)

1. Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

- (i) **Bibi yangu anaishi Kyela.**
- (ii) **Ng'ombe wetu anaitwa Pato.**
- (iii) **Juzi tulicheza mpira uwanjani.**
- (iv) **Samani zina thamani mno.**
- (v) **Babu atanunua kamba ndefu.**

SEHEMU B (Alama 10)

2. Katika kipengele (i) – (v), andika wingi wa maneno yafuatayo kwa kuandika jibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Mto

Wingi wake ni **mito**.

(ii) Ukucha

Wingi wake ni **kucha**.

(iii) Ng'ombe

Wingi wake ni **ng'ombe**.

(iv) Ufa

Wingi wake ni **nyufa**.

(v) Wembe

Wingi wake ni **nyembe**.

SEHEMU C (Alama 10)

3. Andika jibu sahihi kwa maswali yafuatayo.

(i) Bibi hulalamika kila siku anaibiwa fedha zake, siku moja alimkuta Chautundu anaiba fedha zake. Bibi atatumia methali ipi kumsuta Chautundu?

Methali ni **Mwizi hukamatwa kwa pupa**.

Utatumia methali ipi kumhimiza rafiki yako kufanya kazi kwa bidii?

Methali ni **Mtaka cha mvunguni sharti ainame.**

“Samaki mkunje angali mbichi” Methali hii ina maana gani?

Maana yake ni **mtu hufundishwa au hurekebishwa akiwa bado mdogo.**

(ii) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi:

(a) Mdharau mwiba

Methali kamili ni **Mdharau mwiba hujikuta kwenye miba.**

(b) Kilema si

Methali kamili ni **Kilema si umaskini.**

SEHEMU D (Alama 10)

4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa kuandika alama sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Afadhali mgeni amewasili

Afadhali mgeni amewasili!

(ii) Baba ameninunulia kalamu rula na daftari

Baba ameninunulia kalamu, rula na daftari.

(iii) Hodii je wenyeji wangu mpo

Hodii! Je, wenyeji wangu mpo?

(iv) Aka mimi sipendi utoro

Aka! Mimi sipendi utoro.

(v) Mama baba na kaka watasafiri kesho

Mama, baba na kaka watasafiri kesho.

SEHEMU E (Alama 10)

5. Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Hapo zamani za kale Kanga na Kuku walikuwa marafiki sana. Wote waliishi kwa binadamu. Kuku alikuwa na tabia ya uchoyo. Kuku alikuwa na sindano nzuri ya kushonea nguo. Kila siku Kanga alipojaribu kuazima sindano, Kuku alikataa katakata. Siku moja Kanga aliiba sindano ya Kuku akaenda kuificha porini.

Kuku aliporudi aliitafuta sindano yake kila mahali lakini hakuiona. Alianzisha ugomvi mkubwa sana. Wakati wanapigana, Kuku alichukua kalamu mezani kisha akampiga Kanga. Kwa bahati mbaya wino wa kalamu ulivuja mpaka ukaisha. Ndiyo maana hadi leo Kanga ana madoamadoa na Kuku anaparua ardhini kutafuta sindano yake.

Maswali:

(i) Kuku na Kanga waliishi wapi?

Waliishi **kwa binadamu.**

(ii) Nani alikuwa na sindano ya kushonea nguo?

Aliyekuwa na sindano ni **Kuku.**

(iii) Sindano ilipoibiwa ilifichwa wapi?

Ilifichwa **porini.**

(iv) Hadithi hii inahusu nini?

Inahusu **uchoyo na wizi.**

(v) Hadithi hii inatoa funzo gani?

Inatufundisha kwamba **uchoyo na wizi husababisha ugomvi na matatizo.**

